TANGAZO LA SERIKALI NA. 213 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 264 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 6

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 6 kwa-

(a) kufuta kanuni ndogo ya (1) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(1) Halmashauri itahakikisha kwamba ada au ushuru unakusanywa wakati wote katika maeneo yake.";

(b) kufuta kanuni ndogo ya (2); na

(c) kubadili mpangilio wa kanuni ndogo za (3) hadi (5) kuwa kanuni ndogo za (2) hadi (4) mtawalia.

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika katika Jedwali la Kwanza-

(a) katika Sehemu ya 1, kwa kuongeza mara baada ya kipengele cha 3 cha aya B kipengele kipya kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Wanyama wengine | 2,000/= |

(b) katika Sehemu ya 5 – C, kwa kuongeza maneno “kwa kila moja” mara baada ya viwango vya ushuru vilivyoainishwa katika vipengele cha 11, 12, 14, 15 na 16;

(c) katika Sehemu ya 7, kwa-

(i) kufuta neno “lenye“ lililopo katika vipengele vya 1 na 3 na badala yake kuweka maneno “kuanzia Kilo 51 hadi”; na

(ii) kufuta neno “lenye” lililopo katika vipengele vya 2 na 4 na badala yake kuweka neno ‘‘lisilozidi”; na

(d) katika Sehemu ya 9, kwa kufuta maneno “kwa kila baada ya miezi mitatu” kwenye safu ya tatu ya kipengele cha 14 na badala yake kuweka maneno “kwa kila baada ya miezi sita”.

Dodoma,
10 Januri, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*